Septemba 23, mwaka huu. PICHA: STEVEN WILLIAM

USAFIRI

Pg 9 Nipashe Jumatano 24/9/2025

# Madereva waagizwa kuzingatia sheria

**Na Steven William,**

MUHEZA

KIKOSI cha Usalama Barabarani wilayani hapa mkoa wa Tanga, kimewaagiza madereva kuzingatia sheria ili kuepuka ajali, vifo na kupoteza nguvu kazi ya taifa.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Mkuu wa Kikosi hicho wa Wilaya ya Muheza, Leonard Bandola wakati akitoa elimu kwa madereva wa bodaboda, bajaji na guta wilayani hapa.

Bandola, aliwataka madereva hao kuzingatia sheria za usalama barabarani na washauri wa wamiliki wa vyao kufuata taratibu zote za kisheria, ikiwamo kukata bima.

Alisema kikosi hicho kitaendelea kutoa elimu kwa madereva hao kwa lengo la kuwakumbusha kutekeleza majukumu yao ili kudhibiti ajali barabarani, vifo na ulemavu kwa majeruhi.

" Mmekuwa sehemu ya kusababisha ajali kutokana na kudharau sheria za barabarani kwa kujiona mpo juu, " alisema Bandola.

Alisema asilimia 90 ya ajali barabarani, zimekuwa zikisababishwa na baadhi ya madereva kutozingatia sheria za barabarani.

Mkuu wa Jeshi la Polisi wa Wilaya hiyo, Charles Ntenga aliwataka madereva kujiunga na vyuo vya udereva kupata mafunzo na kukabidhiwa leseni.

CamScanner

ELIMU

Rasi Nipashe 3.fano 24/9/2025

# Wadau kudhibiti ajali barabarani kwa wanafunzi

**Na Faustine Feliciane**

WADAU mbalimbali wamekutana jana jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kujadili na kuongeza uelewa kwa umma kuhusu usalama barabarani hususani kwa wanafunzi.

Kikao hicho pia kilishirikisha wataalam wanaohusika na usanifu, ujenzi na ukarabati wa barabara.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana baada ya kikao hicho, Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Amend Tanzania, Simon Kalolo, alisema pia waliwashirikisha wanafunzi kutoka shule za msingi Pius Msekwa, Kunduchi na Tegeta ambazo zote zipo kando ya barabara kubwa.

Alisema shule hizo zinatarajiwa kunufaika na Mradi wa Maendeleo ya Jiji la Dar es Salaam (DMDP 2).

Kupitia majadiliano na wanafunzi hao, mradi ulilenga kukusanya maoni na uzoefu wao kuhusu safari zao za kwenda na kurudi shuleni.

"Mpango huu unaangazia umuhimu wa kushughulikia mahitaji ya watumiaji wa barabara walio hatarini ambao wako katika hatari kubwa. Mjadala huu ni sehemu ya mpango mpana zaidi wa kukuza mtazamo wa 'kuzingatia watu' au 'kuzingatia mtoto' katika ujenzi wa barabara.

"Na kuacha mtindo wa kawaida wa kuyapa kipaumbele magari. Mradi wa DMDP 2, unaofadhiliwa na Benki ya Dunia kwa zaidi ya dola milioni 330, unatazamiwa kuboresha takriban kilomita 260 za barabara kati ya mwaka 2025 na 2030.

"Lengo letu ni kuanzisha jukwaa ambalo watoto wanaweza kubadilishana uzoefu na mitazamo yao na viongozi na wahandisi wanaohusika katika miradi ya barabara," alisema Kalolo.

Alisema kwa kujumuisha mchango wa watoto katika mchakato wa kubuni zinaweza zikajengwa barabara ambazo ni salama na zinazofaa zaidi watembea kwa miguu na watu wenye mahitaji maalumu.

Aliongeza kuwa mpango huo unaungwa mkono na serikali wakiwamo TARURA na Benki ya Dunia (WB), ambao wana nia ya kusimamia uhusiano wa umma kwa ufanisi.

"Ikiwa tutatetea kwa mafanikio ujenzi wa barabara inayolenga watoto, tunaweza kusaidia kuzuia vifo na majeraha mengi miongoni mwa watoto wanaotembea kwa miguu," alisema.

Pia, amesema taasisi hiyo inalenga kutumia vyombo vya habari kuongeza zaidi ufahamu wa usalama barabarani unaozingatia watoto miongoni mwa watunga sera, wataalamu wanaohusika na hatua zote za miradi ya barabarani na umma kwa ujumla.

Agatha Tembo, kutoka mradi wa DMDP-KMC, amesema ushirikiano baina ya wadau wote wa usalama barabarani ni muhimu katika kusaidia kuepusha ajali na wajenzi wakiweka vibao vya mbao wakati wa ujenzi watoto au wazazi wasivichukue kwenda kugeuza kuni majumbani.

Aidha, mwalimu wa Shule ya Msingi Kunduchi, Prosper Lyimo, amesema walimu wawe wanakutana na wanafunzi asubuhi na baada ya masomo ili wawakumbushe hatari zinazoweza kutokea wakati wa ujenzi.

Nipashe Jumatano Septemba 24, 2025 Pg 15

# Polisi wakemea wenye mabasi tiketi za abiria

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

JESHI la Polisi Mkoa wa Singida, limekemea baadhi ya kampuni za mabasi nchini kukata tiketi kwa abiria kinyume na miongozo ya leseni zao na kuwasababishia usumbufu na kuongezeka kwa gharama za safari.

Mkuu wa Opareshenі wa Kikosi cha Usalama Barabarani Tanzania, Joseph Mwakabonga, alikemea tabia hiyo jana wakati akizungumza na baadhi ya madereva wa kampuni hizo katika kituo cha ukaguzi wa magari cha Mizani kilichoko Kata ya Mandewa Wilaya ya Singida mkoani hapa.

Mwakibolwa, alisema jeshi hilo linafanya operesheni hiyo kwa lengo la kutoa elimu kwa abiria, kufanya ukaguzi wa leseni, magari mabovu na mabasi yanayozidisha abiria na kuwachukulia hatua papo kwa papo.

"Kuna tabia iliyozuka ya baadhi ya mabasi kukata tiketi kinyume cha utaratibu wa kisheria, sasa tumeanza operesheni hii ambayo itakuwa endelevu na tukiwakamata wahusika tutachukua hatua," alisema.

Aliwakumbusha abiria kufunga mikanda wakati wote wa safari na kutoa taarifa dereva anapozidisha mwendo au kuvunja sheria za barabarani ili kuwawezesha kusafiri katika hali ya usalama na amani.

Mkuu wa Kikosi hicho wa Mkoa wa Singida, Robert Sewando alitoa rai kwa madereva wanaofanya safari kupitia Singida kujikagua na kijionya vinginevyo atakaevunja sheria kwa makusudi leseni yake itafungwa.

"Tumejipanga kuhakikisha sheria za usalama barabarani zinazingatiwa na madereva wote kwa hiyo yeyote tutakayemkamata akizivunja kuna adhabu kadhaa zitatolewa ikiwamo kunyang'anywa leseni," alisema.